

Tarehe 05.04.2024

**TANGAZO LA ZABUNI YA MATENGENEZO YA MAGARI YA KCU (1990) LTD MSIMU
2024/2025**

Zabuni na: KCU/Z/2024/2025/02

1. KCU (1990) LTD inayo magari yake yanayotumika kwa shughuli mbalimbali za kiofisi, na kwa kuwa magari hayo yanahitaji matengenezo ya mara kwa mara hivyo imetenga fedha kwa ajili ya kuingia makubaliano ya kimkataba na mtoa huduma ya matengenezo ya magari makubwa na madogo kwa msimu 2024/2025.
2. Makampuni/Mashirika/Mtu binafsi yanayotambulika yanakaribishwa kuleta maombi ya zabuni hii ili kutoa huduma ya kutengeneza magari makubwa na madogo ya KCU.
3. Mwombaji awe na leseni ya utengenezaji wa magari makubwa na madogo.
4. Mwombaji awe na Gereji/eneo maalumu la kudumu la kutengeneza magari
5. Mwombaji aeleze uzoefu wa kazi alizowahi kufanya na uwezo wake wa kupata vipuri vya magari, makubwa na madogo.
6. Ombi la zabuni liwe na jina, anuani halisi la mwombaji na mahali Ofisi ilipo. (Physical address)
14. Maombi yaambatane na ada ya TShs. 100,000/= ambazo hazitarejeshwa kwa mwombaji. Fedha hizo zilipwe kupitia A/C Namba **01J1055955001 KAGERA COOPERATIVE UNION (1990) LTD** iliyopo **CRDB**
7. Tathmini itafanywa kwa kuzingatia vigezo 1-7 vilivyo tajwa hapo juu.
8. Barua za maombi zilizofungwa katika bahasha yenye lakiri na kuandikwa juu yake:-
"MAOMBI ZABUNI YA MATENGENEZO YA MAGARI YA KCU MSIMU 2024/2025
kwa anuani tajwa hapa chini,

MENEJA MKUU,
KCU (1990) LTD,
P.O BOX 5,
BUKOBA.

9. Bahasha hiyo iletwe kwa mkono katika ofisi ya manunuzi KCU (1990) Ltd kabla au mnamo tarehe 19.04.2024. saa 4.00 asubuhi siku ya Ijumaa na ufunguzi wa maombi yote utafanyika muda huo, waombaji au wawakilishi wa waombaji wanaalikwa katika ufunguzi mara tu baada ya saa ya mwisho yakupokea zabuni.
10. Maombi yatakayo chelewa, maombi yasiyokamilika, maombi yaliyowasilishwa kwa njia ya kieletroniki na maombi yasiyokuwepo siku ya ufunguzi hayatahusishwa na uchambuzi wa kumpata mzabuni.
Imetolewa na;

MENEJA MKUU
KCU (1990) LTD

